# MAHAFALI YA 18 YA CHUO CHA UFUNDI ARUSHA

Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha anawatangazia wahitimu, wanafunzi, watumishi, Wazazi/ walezi na wadau wote Chuo, kuwa mahafali ya 18 ya Chuo cha Ufundi Arusha yatafanyika siku ya **Alhamisi tarehe 12 Novemba, 2026** kampasi kuu iliyopo jiji la Arusha.

Mahafali haya yatatanguliwa na sherehe ya **kusanyiko (Convocation Ceremony)** itakayofanyika siku ya **Jumatano tarehe 11 Novemba, 2026**. Pia sherehe ya kusanyiko (Convocation Ceremony) itatumika kutambua na kuwatunukia zawadi wanafunzi wote waliofanya vizuri katika masomo yao.

Kufuatia tangazo hili, wahitimu wote wanaombwa kuhakiki majina yao na taarifa nyingine muhimu kupitia tovuti ya Chuo **(www.atc.ac.tz).** Ma jina ya wahitimu yatapatikana kwenye tovuti kuanzia **siku ya Jumatano tarehe 9 Septemba, 2026** Kwa wale wenye marekebisho wanahimizwa kutuma taarifa zao

kupitia anuani ya barua pepe registrar@atc.ac.tz yenye kichwa cha habari **'UHAKIKI WA MAJINA YA WAHITIMU** Mwisho wa kutuma marekebisho ni **Jumatatu, tarehe 14 Septmba, 2026.**

Aidha, wahitimu wote wanaombwa kuthibitisha ushiriki wao kwenye mahafali hayo kupitia anuani ya barua pepe **registrar@atc.ac.tz.**

**Wahitimu wanaombwa kulipia Majoho kwa kiasi cha TZS 50,000/- kwa kutumia control number inayopatikana kwenye tovuti ya Chuo.**

Tafadhali, upatapo tangazo hili mtaarifu na mwenzako.

Mkuu wa Chuo anawatakia maandalizi mema.

**Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Masko- Chuo cha Ufundi Arusha**